**Wito wa insha: Sheria linganishi ya mali, iliyojikwamua kutoka kwenye ukoloni**

*Novemba 4-6 2024 huko Brasília (Brazili)*

Mwisho wa kuwasilisha insha: Februari 14, 2024

Maamuzi: Aprili 14, 2024

**MADA:** kufuatia warsha kuhusu methodolojia (Witwatersrand 200) na sheria kabla ya ujio wa ukoloni (Oxford 2022), warsha ya tatu ya sheria linganishi ya mali, iliyojikwamua kutoka kwenye ukoloni itakayofanyika Brasilia itajikita katika mbinu zilizojikwamua kutoka ukoloni kwa sheria linganishi ya sheria ya mali. Mali ni ya umuhimu mkubwa katika sheria linganishi ya mali, iliyojikwamua kutoka kwenye ukoloni. Dhana nyingi kuhusu sheria ya mali katika mataifa ya Kaskazini mwa ulimwengu – kwa mfano nadharia ya kazi katika mali ya John Locke – iliibuka kutoka kwenye muktadha wa kikoloni. Kadhalika, ukoloni-mamboleo (katika muundo, kwa mfano, wa ubepari wa taka) unaendelea kuathiri mali binafsi na za umma katika nchi za Kusini mwa Ulimwengu. Pia, hali ya ukoloni inaeneza dhana ya mali kama nafasi binafsi ya uhuru; dhana hii inaondoa dhana mbadala, zisizo za mataifa ya Kaskazini mwa ulimwengu, kwa mfano umiliki wa jumuiya, usimamizi, au utu wa mito na milima.

Warsha yetu inalenga kujiondoa kwenye dhana za kikoloni kuhusu mali, umiliki na milki, huku ikitambua pia ugiligili na wingi (wa kihistoria na zama hizi) wa sheria katika mataifa ya Kusini mwa ulimwengu (kimila, kiasili, au vinginevyo). Kupitia ukosoaji wa sheria za mali za zama hizi ambazo zinatambua mahusiano yake na ukoloni na jinsi inavyoendelea hali ya ukoloni, tunahimiza matumizi ya uondoaji ukoloni katika kesi za sheria linganishi za mali, hususan katika mlingano baina ya mataifa ya Kusini mwa Ulimwengu. Japo tunatambua kutoweza kutenganisha mali binafsi na mali ya umma na umuhimu wa mamlaka ya nchi kwa dhana ya mali, hatutaki kurudia tu ukosoaji dhidi ya sheria za kimataifa zilizopo kuhusu mada hizi. Tunatarajia kuchunguza aina zilizojitenga na ukoloni za milki (yaani, kufuta umiliki binafsi, haki ya jiji) na tafsiri zilizojitenga na ukoloni zilizopo mataifa ya kusini mwa ulimwengu na sheria ya mali ya asili. Kuliko kutambua tu sheria ya kikoloni ya mali, tunakaribisha insha ambazo zitazungumzia mitazamo iiliyojietenga na ukoloni, za asili na zisizo za kikoloni kuhusu mali

Insha zitakazochaguliwa aidha zitajikita katika sheria ya mali ya asili au ya makundi madogo katika jamii, au dhana nyingi za sheria ya mali ambayo inaunganisha sheria ya kabla ya ujio wa ukoloni na kuendana na hali kwa kila siku kuhusiana na zama za sasa.

Mada zinaweza kuwa pamoja na: dhana za asili na zisizo za kikoloni kuhusu mali na mahusiano kwa dunia isiyo na uhai; fursa isiyo na kikoloni na ya asili kwa ardhi na maliasili (kwa mfano maji); uelewa wa asili kama mali; tofauti kati ya umiliki na milki; athari za kisheria za kutoondosheka kwa ardhi na asili; uhusiano kwa ardhi na maji ambao unatofautiana na dhana ya kitenda-kitendwa katika mali.

Tunakaribisha insha zitakazoyumbisha hali ya ukoloni kwa kujikita kwenye kwanini na kwa vipi jamii za asili na mataifa ya kusini mwa ulimwengu yanatafsiri au kutenda sheria ya mali na milki, au kinyume chake.

**KUWASILISHA INSHA:** Insha shurti ziwe zimetokana na utafiti halisi (itapendeza ikiwa utategemea vyanzo vya msingi au vya asili) na kwenye mbinu zilizojikwamua kutoka kwa ukoloni za sheria linganishi. Insha shurti zibainishe "sheria ya mali" katika tamaduni au sehemu mahususi, na mkazo kamili kwa mbinu na utendaji uliojitenga na ukoloni, asili na kabla ya ukoloni. Waandishi wanahimizwa kutumia bibliografia kuhusu dhana ya kujitenga na ukoloni na stadi zilizojitenga na ukoloni za sheria zinazopatikana katika tovuti ya Mradi wa DeCoLa. Upendeleo utatolewa kwa insha ambazo ni linganishi na zinajikita moja kwa moja katika insha za kisomi zilizopo. Tafadhali tuma insha yako kwa wingu letu salama (i) kama

kiambatanisho katika kiolezo kilichotolewa na tovuti ya Mradi wa Sheria Linganishi ya mali, iliyojikwamua kutoka kwenye ukoloni (ii) katika lugha yoyote (iii) isiyozidi maneno 5,000 (iv) mwisho ni tarehe 14 Februari 2024. Utapokea kwa baruapepe uthibitisho kupokelewa kwa chapisho lako.

**MAPITIO YA RIKA:** Bodi ya ushauri ya mapitio ya rika inawajumuisha Ahmad Amara (NYU Tel Aviv; Chuo Kikuu cha Ben Gurion), Roberta Caminero Bagiio (Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Rio Grande do Sul - UFRGS), Isidore Leopold Miendjiem (Chuo Kikuu ha Dschang), na Ambreena Manji (Chuo Kikuu cha Cardif).

**INSHA ZITAKAYOKUBALIKA:** Waandishi wa insha zitakazokubalika watapata fursa ya kuwasilisha matoleo yaliyohaririwa kwa ajili ya warsha. Insha zitakazowasilishwa ambazoo zitakuwa katika lugha tofauti na Kiingereza zitatafsiriwa kitaalamu. Insha zitasambazwa kabla ya warsha; waandishi hawatowasilisha insha zao wakati wa warsha. Baada ya mapito ya rika, insha zitachapishwa kwenye juzuu iliyohaririwa au katika toleo la jarida la kongamano.

**RATIBA:**

| | |
|---|---|
| Februari 14, 2024 | tarehe ya kuwasilisha rasimu ya insha |
| Aprili 14, 2024 | kukubaliwa au kukataliwa |
| Juni 14, 2024 | tarehe ya kuwasilisha rasimu ya insha iliyohaririwa |
| Novemba 4-6, 2024 | kuwasilisha insha ana kwa ana na majadiliano kuhusu insta huko Brasilia |
| Januari 10, 2025 | tarehe ya mwisho ya kuwasilisha insha kamili |

**WAANDAAJI WENZA:** Warsha hii ya tatu inaandaliwa kwa pamoja na Mradi wa DeCoLa uliopo katika Taasisi ya Max Plank ya Sheria Linganishi na ya Kimataifa ya Mali (MPIPriv) huko Hamburg na Mtandao wa Kujiondoa kwenye Ukoloni na Kulinganisha Uzoefu wa Kisheria (DECLEN) katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Brasilia. Mradi wa DiCoLa unaongozwa na Ralf Michaels (MPIPriv). Kwamou Eva Feukeu (MPIPriv) ni mratibu wa mradi wa DeCoLa. DECLEN is mtandao wa kisomi unaoendeshwa kwa pamoja na Deo Campos Santos na Guilherme Borges (Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Brasilia).

**MAHALI**: Warsha itafanyika katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Brasilia na itajumuisha maongezi ya kijamii na wanaharakati wa Brazili na majadiliano ya mada mbalimbali kuhusu mali. Huduma za kutafsiri zinaweza kutolewa.

**UFADHILI:** MPRriv inaweza kutoa ufadhili kwa washiriki wa kimataifa kwenye warsha. Waandaaji wanatarajia kutoa malazi ya usiku tatu huko Brasilia na marejesho ya gharama za usafiri kwa waandishi wa insha zitakazokubaliwa.

**UTARATIBU:** Warsha itafuatiwa na shule ya majira ya kuchipuka itakayofanyika katika Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Bahia Novemba 7 hadi 9, 2024. Warsha na shule ya msimu wa kuchipuka zinaratibiwa na kamati ya utaratibu, ambayo inawajumuisha Anna Lyvia Ribeiro (Kamisheni Maalum ya Sheria za Biashara ya ardhi na majengo), André Nunes Chaib (Chuo Kikuu cha Maastricht), Fernanda Frizzo Bragato (Shule ya Sheria ya Unisinos – UNISINOS), Flavia Carlet (Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Rio de Janeiro – UFRJ), Karina Gomes Machado (Shule ya Sheria ya Unisinos – UNISINOS), Luiz Eduardo de Lacernda Abreu (Chuko Kikuu cha Brasilia – UNB), na Tatiana Emilia Dias Gomes ( Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Bahia – UFBA).

**WASILIANA NA:** decolonial@mpipriv.de